


Modern Churches Timeline

Tangu Agano Jipya mpaka leo



Pamoja na makumi elfu ya makanisa na madhehebu tofauti, yakiwa na imani na matendo yanayopingana katika ulimwengu wa leo, mara nyingi tunabaki tukiwa tumechanganyikiwa. Je, ni kanisa lipi lililo kanisa "sahihi?" Je, ni kanisa lipi analolikubali Mungu? Je, ni kanisa lipi lililoanzishwa na Kristo? Katika Mdo. 2, tunasoma kuhusu kanisa moja la kweli ambalo lilianzishwa na Yesu Kristo na kuwekwa wakfu na Mungu. Makundi mengi ya kidini yameliacha lile kanisa la karne ya kwanza, yakitawanyika katika makanisa na madhehebu mbalimbali tuyaonayo leo. Kama tunatafuta kuwa kanisa moja la kweli lililoanzishwa na Yesu Kristo kwenye karne ya kwanza, kama ilivyoelezewa katika Mdo. 2, ni lazima tuzitoe nafsi zetu katika vitabu vya miongozo, mafundisho na mapokeo yaliyotengenezwa na wanadamu, na kufanyika kuwa kanisa la karne ya kwanza tunalolisoma kwenye Agano Jipya.